Tawhiyd-ul-Mursaliyn wa waa yudhwaaddihaa minal-Kufri wash-Shirk

[Tawhiyd ya Mitume na zile kufuru na shirki vinavyopingana nayo]

Mwandishi:

Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz

Tarjama:

Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush

YALIYOMO:

01. Lengo la kutumwa Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam)....4
02. ´Ibaadah ndio Tawhiyd....6
03. Maana ya Twaaghuut....9
04. Ndio maana washirikina wa kale walikataa kutamka Shahaadah....10
05. Lengo la kuteremshwa vitabu na historia ya baadhi ya Mitume walivyopambana kwa ajili ya Tawhiyd.13
06. Allaah ndiye ananufaisha duniani na kuokoa Aakhirah....20
07. ´Ibaadah ni haki ya Allaah peke yake....22
08. Muusa na Haaruun walivyotumwa kumlingania Fir´awn....24
09. Muusa alimweleza Fir´awn ya kwamba Allaah yuko juu mbinguni....27
10. Wafuasi wa ´Iysaa wanamtambua Allaah zaidi kuliko Jahmiyyah na vifaranga vyao....28
11. Kuna Aayah nyingi zinazothibitisha kuwa Allaah yuko juu ya mbingu....30
12. Baadhi ya sifa za Allaah zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah....31
13. Sifa za viumbe hazifanani na sifa za Allaah kwa njia yoyote ile....33
14. Mfumo wa Ahl-us-Sunnah katika kuthibitisha majina na sifa za Allaah....35
15. Ndio maana ndama hakustahiki kuabudiwa....36
16. Ndio maana Allaah akastahiki kuabudiwa....37
17. Kazi kubwa waliokuwa nayo Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam)....38
18. Tawhiyd kwanza....40
19. Namna waarabu walivyobadilishiwa dini yao....41
20. Mtume na Maswahabah wake kuhajiri al-Madiynah kukimbia maudhi ya Quraysh....43
21. Chanzo cha kujitokeza shirki na kubainisha kwamba Nuuh ndiye Mtume wa kwanza....44
22. Idadi ya Mitume na Manabii haitambuliki....46
23. Maudhi yaliyompata Mtume na watu wake kwa sababu ya Tawhiyd....47
24. Lengo la kuteremshwa Vitabu....48

25. Uchambuzi wa aina za Tawhiyd 49

26. Msimamo wa washirikina wa kale na wa sasa juu ya Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah.....52

27. Uwajibu wa kupupia kulingania na kueneza kheri 54

01. Lengo la kutumwa Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam)

Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu. Mwisho mwema ni kwa wachaji. Swalah na salaam ziwe juu ya kiongozi wa [watu] wa mwanzo na wa mwisho, Manabii na Mitume wengine wote na kila mwema.

Amma ba´d:

Ilipokuwa kumpwekesha Allaah (´Azza wa Jall), kumuamini Yeye na Mitume Wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) ndio wajibu ulio muhimu zaidi na faradhi ilio kubwa na kuyatambua hayo ndio elimu tukufu na ilio bora zaidi na ilipokuwa haja ya msingi huu mkubwa inapelekea kuubainisha kwa upambanuzi ndipo nikaonelea kuliweka wazi katika maneno haya mafupi kutokana na haja kubwa ya hilo. Maudhui hii kubwa inatakiwa kutiliwa umuhimu mkubwa. Ninamuomba Allaah (´Azza wa Jall) atuwafikishe sisi sote kuifuata haki katika maneno na vitendo na atukinge sote kutokamana na makosa na kuteleza. Nasema na huku nikimuomba Allaah msaada na mafanikio:

Hapana shaka kwamba Tawhiyd ndio wajibu ulio mkubwa kabisa, ndio faradhi ya kwanza kabisa, ndio ulinganizi wa Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) na ndio lengo la ulinganizi huu. Hivyo ndivyo amebainisha Mola wetu (´Azza wa Jall) katika Kitabu Chake kinachoweka wazi na Yeye ndiye mkweli wa wasemaji. Amesema (Subhaanahu wa Ta´ala) kuhusu Mitume wote:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

“Hakika Tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: “Mwabuduni Allaah na jiepusheni na Twaaghuut.”” (16:36)

Amebainisha (Jalla wa ´Alaa) ya kwamba ameutumia kila Ummah Mtume akiwaeleze wamwabudu Allaah na wajiepushe na *Twaaghuut*. Huu ndio ulikuwa ulinganizi wa Mitume wote ambapo kila mmoja alikuwa akiwaambia watu wake na Ummah wake wamwabudu Allaah na wajiepushe na *Twaaghuut*. Maana yake ni kwamba wamuabudu Allaah peke yake. Kwa kuwa ugomvi kati ya Mitume na nyumati ilikuwa ni Tawhiyd-ul-Uluuhiyyah. Vinginevyo ni kwamba nyumati zilikuwa zikikubali ya kwamba Allaah ndiye Mola wao, muumbaji wao, mruzukaji wao na wakitambua sifa na majina Yake mengi. Mizozo na ugomi, tangu wakati wa Nuuh mpaka wakati wetu huu ni katika Tawhiyd-ul-Uluuhiyyah. Mitume walikuwa wakiwaambia watu wamwabudu Allaah na wamtakasie Yeye ´ibaadah na waache kuwaabudu wengine. Upande wa pili maadui na wapinzani wao wakiwaambia kwamba watamwabudu na wakati huo huo wawaabudu wengine na kwamba hawawezi kumkhusisha Yeye pekee kwa ´ibaadah. Hapa ndipo palipokuwa mgogoro kati ya Mitume na watu wao. Msingi ni kwamba watu wao walikuwa hawapingi kumuabudu. Mzozo ulikuwa kama wamwabudu Yeye peke yake au wasimwabudu Yeye peke yake.

Allaah amewatuma Mitume ili wamkhusishe Mola kwa ´ibaadah na wampwekeshe kwayo pasi na wengine. Hilo ni kwa sababu Yeye (´Azza wa Jall) ndiye mfalme, muweza juu ya kila jambo, muumbaji, anayewaruzuku waja, mjuzi wa hali zao na mengineyo.

02. ´Ibaadah ndio Tawhiyd

Kwa ajili hii ndio maana Mitume wote (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) waliziita nyumati zao katika kumpwekesha Allaah, kumtakasia Yeye ´ibaadah na kuacha kuabudu vinginevyo. Hii ndio maana ya maneno Yake (´Azza wa Jall):

اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

Ibn ´Abbaas (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesema kuhusu maana hii:

"´Ibaadah ndio Tawhiyd."

Hivi ndivyo walivyosema wanachuoni wote ya kwamba ´ibaadah ndio Tawhiyd. Kwani hilo ndio lengo. Nyumati zilizotangulia zilikuwa zikimwabudu Allaah na wakati huo huo zikiwaabudu wengine. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ

"Pindi Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: "Hakika mimi ni mwenye kujitenga mbali kabisa na yale mnayoyaabudu - isipokuwa ambaye ameniumba, basi hakika Yeye ataniongoa."" (43:26-27)

Akajitenga mbali na waungu wao isipokuwa Muumbaji Wake (Subhaanah). Ikatambulika kuwa walikuwa wakimwabudu Yeye na wakati huo huo wakiabudu pamoja Naye wengine. Kwa ajili hii ndio maana Ibraahiym alijitenga na waungu wao mbali isipokuwa Muumbaji Wake (´Azza wa Jall) ambaye ni Yeye Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَأَعْتَزِلُكُمْ وَمَا تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ وَأَدْعُو رَبِّي

"Nakutengeni na vile mnavyoviomba pasi na Allaah na namuomba Mola wangu." (19:48)

Ikatambulika kuwa walikuwa wakimuabudu Allaah na wakiwaabudu wengine. Aayah zilizo na maana kama hii ni nyingi. Kwa hivyo tukatambua malengo ya ulinganizi wa Mitume na kumkhusisha Allaah kwa ´ibaadah na kumpwekesha kwayo. Kwa msemo mwingine asiombwe yeyote isipokuwa Yeye (Jalla wa ´Alaa), hakuombwi uokozi kwa mwingine isipokuwa Kwake, hakuwekwi nadhiri kwa mwingine isipokuwa Kwake, hakuchinjwi kwa ajili ya mwingine isipokuwa Yeye, haswaliwi mwingine isipokuwa Yeye na ´ibaadah nyenginezo zote. Yeye ndiye anayastahiki (Jalla wa ´Alaa) pasi na mwengine. Hii ndio maana ya "Hapana mungu isipokuwa Allaah". Maana yake ni kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Hii ndio maana yake kwa wanachuoni. Kwa kuwa waungu waliyopo ni wengi na washirikina tangu hapo kale wakati wa Nuuh walikuwa wakiabudu waungu badala ya Allaah. Miongoni mwa waungu hao ilikuwa ni Wadd, Suwaa´, Ya´uuq, Nasr na wengineo. Waarabu walikuwa na waungu wengine wengi. Wafursi na warumi pia walikuwa na waungu wengi ambao walikuwa wakiwaabudu pamoja na Allaah. Ndipo ikatambulia kuwa makusudio ya "Hapana mungu isipokuwa Allaah" ndio malengo ya ulinganizi wa Mitume ambao ilikuwa ni kumuabudu Allaah peke yake na kumkhusisha kwa ´ibaadah pasi na wengine wote. Kwa ajili hii ndio maana amesema (Subhaanah) katika Kitabu Chake kinachoweka wazi:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ

"Hivyo ni kwa kuwa Allaah ndiye wa haki na kwamba vile [makafiri] wanavyoomba badala Yake ndiyo batili." (22:62)

Hayo yakaweka wazi ya kwamba malengo ni kumkhusisha kwa ´ibaadah pasi na wengine wote na kwamba Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye mwabudiwa wa haki (Jalla wa ´Alaa) na kwamba vile vyote vinavyoabudiwa badala Yake ni vyenye kuabudiwa kwa batili. Kwa ajili hii ndio maana amesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

Bi maana wampwekeshe Allaah na wajiepushe na *Twaaghuut.* Kwa msemo mwingine waache kuabudu *Twaaghuut* na wajitenge nayo mbali.

03. Maana ya Twaaghuut

Twaaghuut ni kila chenye kuabudiwa badala ya Allaah katika watu, majini, malaika na viumbe vyenginevyo midhali hachukii na anaridhia. Makusudio ni kwamba *Twaaghuut* ni kila chenye kuabudiwa badala ya Allaah katika vitu visivyokuwa na uhai na vinginevyo katika vile vinavyoridhia hayo. Kuhusu wale wasioridhia hayo kama vile malaika, Mitume na waja wema *Twaaghuut* katika hali hii atakuwa ni shaytwaan ambaye amewaita kuwaabudu na akawapambia watu.

Mitume, Manabii, malaika na kila mja mwema haridhii kamwe kuabudiwa badala ya Allaah. Kinyume chake wanayakemea hayo na wakayapiga vita. Katika hali hii wao sio *Twaaghuut*. *Twaaghuut* ni kila mwenye kuabudiwa badala ya Allaah miongoni mwa wale wenye kuridhia hayo kama mfano wa Fir´awn, Ibliys na mfano wao katika wale wenye kuita katika hayo au akayaridhia. Vilevile vitu visivyokuwa na uhai katika miti, mawe na masanamu vinavyoabudiwa badala ya Allaah. Vyote hivi vinaitwa *Twaaghuut* kwa sababu ya kuabudiwa badala ya Allaah.

04. Ndio maana washirikina wa kale walikataa kutamka Shahaadah

Aamesema (Subhaanahu wa Ta´ala):

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

"Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimfunulia Wahy ya kwamba: "Hakika hapana mungu wa haki isipokuwa Mimi - basi niabuduni!"" (21:25)

Aayah hii ni kama Aayah zingine zilizotangulia. Ndani yake amebainisha (Subhaanah) ya kwamba ulinganizi wa Mitume wote ilikuwa katika Tawhiyd na kumtakasia ´ibaadah Allaah (Jalla wa ´Alaa) peke yake pasi na wengine wote. Lau ingelikuwa kutamka "Hapana mungu isipokuwa Allaah" kunatosheleza pasi na kutazama kitendo cha kumtakasia Allaah ´ibaadah na kuamini kuwa Yeye ndiye mwenye kuiistahiki basi watu wasingelijizuia kufanya hivo. Lakini washirikina walielewa kwamba kulisema kwao kutabatilisha waungu wao na maneno yao yatapelekea kwamba Allaah ndiye mwenye kuabudiwa kwa haki na mwenye kukhusika juu ya hilo (Jalla wa ´Alaa). Kwa ajili hii ndio maana walilikataa, wakalijengea uadui na wakawa na jeuri kuliitikia. Kwa haya ikapata kuwa wazi ya kwamba malengo ya ´ibaadah ni kumkhusisha Allaah kwa ´ibaadah na kumpwekesha badala ya Mitume, Malaika, waja wema, majini na wengine wote wanaoabudiwa badala Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Kwa kuwa Allaah (Subhaanah) ndiye mfalme, mruzukaji, muweza, muhuishaji, mfishaji, muumbaji wa kila kitu na ambaye anayaendesha mambo yote ya waja. Kwa hiyo Yeye ndiye anayestahiki kuabudiwa na Yeye ndiye mjuzi wa hali zao (Subhaanahu wa Ta´ala). Kwa ajili hiyo ndio maana akawatuma Mitume ili wawalinganie viumbe katika kumpwekesha, kumtakasia Yeye ´ibaadah, kubainisha majina na sifa Zake na kwamba Yeye ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa na kuadhimishwa kwa sababu ya ukamilifu wa elimu, uwezo, majina na sifa Zake. Sababu nyingine ni kwa kuwa Yeye (´Azza wa Jall) ndiye Mwenye kunufaisha, Mwenye kudhuru, mtambuzi wa hali za waja Wake, ni mwenye kuyasikia maombi yao

na ndiye mdhamini wa maslahi yao. Yeye (Jalla wa ´Alaa) ndiye anayestahiki kuabudiwa pasi na wengine wote.

Amekhabarisha (Subhaanah) kuhusu Nuuh, Huud, Swaalih na Shu´ayb (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) ya kwamba waliwaambia watu wao:

اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُ

“Mwabuduni Allaah, kwani hamna mwabudiwa wa haki mwingine asiyekuwa Yeye.” (07:59)

Aayah hii inaenda sambamba na maneno Yake (Ta´ala):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

Watu wa Huud walimjibu Mtume wao (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa kumwambia:

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا

“Wakasema: “Je, umetujia ili tumwambudu Allaah pekee na tuache yale waliyokuwa wakiabudu baba zetu?”” (07:70)

Walielewa vyema ya kwamba maana ya wito wa Huud (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) unapelekea kumtakasia ´ibaadah Allaah peke yake na kuachana na mizimu inayoabudiwa badala Yake. Kwa ajili hii ndio maana walisema:

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا

“Wakasema: “Je, umetujia ili tumwambudu Allaah pekee na tuache yale waliyokuwa wakiabudu baba zetu?”” (07:70)

Matokeo yake wakaendelea juu ya ukaidi wao na kukadhibisha mpaka ikawateremkia adhabu. Tunamuomba Allaah afya.

05. Lengo la kuteremshwa vitabu na historia ya baadhi ya Mitume walivyopambana kwa ajili ya Tawhiyd

Allaah (Subhaanah) ameteremsha vitabu na akawatuma Mitume ili aabudiwe Yeye peke yake hali ya kuwa hana mshirika na haki Yake ibainishwe kwa waja na watajiwe waja yale majina Yake mazuri kabisa na zile sifa Zake kuu mno anazisifika kwazo ili wamtambue (Jalla wa ´Alaa) kwa majina Yake na sifa Zake, ukubwa wa wema Wake, ukubwa wa uwezo Wake na ilivyoenea elimu Yake (Jalla wa ´Alaa). Hilo si kwa jengine isipokuwa ni kwa sababu Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah ndio msingi wa Tawhiyd-ul-Ilaahiyyah na Tawhiyd-ul-´Ibaadah. Kwa ajili hii akawatuma Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam), kukateremshwa vitabu vya kimbingu kutoka kwa Allaah (´Azza wa Jall) kwa ajili ya kubainisha sifa na majina Yake na ukubwa wa wema Wake na vilevile kubainisha kule kustahiki Kwake kuabudiwa, kuadhimishwa na kuombwa (Jalla wa ´Alaa). Lengo ni watu waweze kumuabudu, kumtii, kutubia Kwake na wamuabudu badala ya wengine wote. Haya yanapatikana kwa wingi katika Qur-aan. Allaah (Subhaaahu wa Ta´ala) ameyataja hayo kutoka kwa Mitume Wake wengi (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) pale aliposema:

قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِي اللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Mitume wao wakasema: “Je, kuna shaka juu ya Allaah ambaye ndiye mwanzilishi wa mbingu na ardhi?”” (14:10)

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَا قَوْمِ إِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُم مَّقَامِي وَتَذْكِيرِي بِآيَاتِ اللَّهِ فَعَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْتُ فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوا إِلَيَّ وَلَا تُنظِرُونِ

“Wasomee habari ya Nuuh alipowaambia watu wake: “Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu na kukumbusha kwangu Aayah za Allaah kunakutieni mashaka, basi kwa Allaah nategemea; basi pangeni jambo lenu na washirika wenu kisha jambo lenu lisifichike kwenu halafu mpitishe kwangu wala msinipe muhula.” (10:71-72)

Akabainisha (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ya kwamba yeye ni mwenye kumtegemea Allaah (Jalla wa ´Alaa) na kwamba hajali vitisho na kumtia kwao

khofu na kwamba ni wajibu kwake kufikisha ujumbe wa Allaah, jambo ambalo alilifanya kweli (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) na akawatambuza uwezo na ukubwa wa Mola wake, kwamba ni Mwenye kukizunguka kila kitu, muweza wa kuwaokoa, kuwaangamiza maadui Wake kama ambavyo vilevile ni muwezo wa kuwalinda Mitume na Manabii Wake, kuwazunguka kwa kuwalinda na kuwasaidia juu ya kufikisha ule ujumbe waliokuja nao. Akateremsha kuhusu haya Suurah inayohusiana na Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pale aliposema:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ إِنَّا أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ أَنْ أَنذِرْ قَوْمَكَ مِن قَبْلِ أَن يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ قَالَ يَا قَوْمِ إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ وَأَطِيعُونِ يَغْفِرْ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخِّرْكُمْ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ أَجَلَ اللَّهِ إِذَا جَاءَ لَا يُؤَخَّرُ ۖ لَوْ كُنتُمْ تَعْلَمُونَ قَالَ رَبِّ إِنِّي دَعَوْتُ قَوْمِي لَيْلًا وَنَهَارًا فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَائِي إِلَّا فِرَارًا وَإِنِّي كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوا أَصَابِعَهُمْ فِي آذَانِهِمْ وَاسْتَغْشَوْا ثِيَابَهُمْ وَأَصَرُّوا وَاسْتَكْبَرُوا اسْتِكْبَارًا ثُمَّ إِنِّي دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ثُمَّ إِنِّي أَعْلَنتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ لَهُمْ إِسْرَارًا فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ إِنَّهُ كَانَ غَفَّارًا يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُم مِّدْرَارًا وَيُمْدِدْكُم بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَيَجْعَل لَّكُمْ جَنَّاتٍ وَيَجْعَل لَّكُمْ أَنْهَارًا مَّا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا

"Kwa jina la Allaah, Mwingi wa huruma, Mwenye kurehemu. Hakika Sisi tumemtuma Nuuh kwa watu wake kwamba: waonye watu wako kabla haijawafikia adhabu iumiazyo. Akasema: "Enyi watu wangu! Hakika mimi kwenu ni mwonyaji mwenye kuweka wazi; kwamba mwabuduni Allaah, na mcheni na mnitii. Atakusameheni madhambi yenu, na atakuakhirisheni mpaka muda maalum uliokadiriwa - hakika muda uliokadiriwa na Allaah utakapokuja hautoakhirishwa iwapo kama mtakuwa mnajua." [Nuuh] akasema: "Mola wangu! Hakika mimi nimewalingania watu wangu usiku na mchana. Lakini haikuwazidishia wito wangu jengine zaidi ya kukimbia. Na hakika mimi kila nilipowaita ili uwasamehe, huweka vidole vyao masikioni mwao na wakagubika nguo zao na wakashikilia wakatakabari kikweli kweli. Kisha hakika mimi niliwalingania kwa waziwazi. Halafu hakika mimi nikawatangazia na nikawasemesha kwa siri. Nikasema: "Mtakeni msamaha Mola wenu, kwani hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe, [endapo mtafanya hivo] atakutumieni mvua tele ya kuendelea, na atakuongezeeni mali na wana na atakupeni mabustani na atakupeni mito" - mna nini nyinyi hamtaraji na hamkhofu taadhima ya Allaah? Na hali amekuumbeni hatua baada ya hatua?" (71:01-14)

Akaweka wazi (Subhaanah) kupitia kwa Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baadhi ya sifa Zake na kwamba Yeye ndiye anawatunuku riziki, kheri tele na neema mbalimbali na kwamba Yeye ndiye anastahiki kuabudiwa,

kutiiwa na kuadhimishwa (Jalla wa ´Alaa). Amesema vilevile kuhusu Huud (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na watu wake katika Suurah "ash-Shu´araa´":

كَذَّبَتْ عَادٌ الْمُرْسَلِينَ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ هُودٌ أَلَا تَتَّقُونَ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّ الْعَالَمِينَ أَتَبْنُونَ بِكُلِّ رِيعٍ آيَةً تَعْبَثُونَ وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ وَإِذَا بَطَشْتُم بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ وَاتَّقُوا الَّذِي أَمَدَّكُم بِمَا تَعْلَمُونَ أَمَدَّكُم بِأَنْعَامٍ وَبَنِينَ وَجَنَّاتٍ وَعُيُونٍ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ

"Kina 'Aad waliwakadhibisha wajumbe. Alipowaambia ndugu yao Huud: "Je, hamchi? Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu, hivyo basi mcheni Allaah na nitiini. Na wala sikuombeni ujira wowote juu yake - ujira wangu hauko isipokuwa kwa Mola wa walimwengu." Je, mnajenga katika kila sehemu maarufu za mnyanyuko, majengo marefurefu kwa ajili ya burudani tu na mnafanya mangome madhubuti kama kwamba mtaishi milele? Na mnapokamata kushambulia mnatumia nguvu kwa uadui na ujabari! Basi mcheni Allaah na nitiini. Mcheni ambaye amekupeni yale mnayoyajua; amekupeni wanyama wa mifugo na watoto na mabustani na chemchemu. Hakika mimi nakukhofieni adhabu ya Siku kubwa." (26:123-135)

Allaah (Jalla wa ´Alaa) akaweka wazi kupitia kwa Mtume wao Huud (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zile neema nyingi alizowaneemesha na kwamba Yeye ndiye Mola wa wote na kwamba ni wajibu kwao kumnyenyekea, kuwatii na kuwasadikisha Mitume Wake. Lakini hata hivyo wakakataa na wakafanya jeuri na adhabu ya upepo mkali ikawa imewateremkia. Amesema kuhusu Swaalih (´alayhis-Salaam):

كَذَّبَتْ ثَمُودُ الْمُرْسَلِينَ إِذْ قَالَ لَهُمْ أَخُوهُمْ صَالِحٌ أَلَا تَتَّقُونَ إِنِّي لَكُمْ رَسُولٌ أَمِينٌ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ وَمَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَىٰ رَبِّ الْعَالَمِينَ أَتُتْرَكُونَ فِي مَا هَاهُنَا آمِنِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ وَزُرُوعٍ وَنَخْلٍ طَلْعُهَا هَضِيمٌ وَتَنْحِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا فَارِهِينَ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ وَلَا تُطِيعُوا أَمْرَ الْمُسْرِفِينَ الَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ

"Kina Thamuud walimkadhibisha wajumbe. Alipowaambia ndugu yao Swaalih: "Je, hamchi? Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu, hivyo basi mcheni Allaah na nitiini. Na wala sikuombeni ujira wowote juu yake - ujira wangu hauko isipokuwa kwa Mola wa walimwengu. Je, mtaachwa mkiwa katika amani kwenye haya hapa mliyonayo; katika mabustani na chemchemu, na mimea na mitende makole yake laini yamewiva? Na

mnachonga majabali ni nyumba kwa uhodari kabisa? Basi mcheni Allaah na nitiini na wala msitii amri ya wenye kupindukia mipaka; wale ambao wanafanya ufisadi katika ardhi na wala hawatengenezi." (26:141-152)

Swaalih (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akabainisha yanayohusiana na Allaah ya kwamba Yeye ndiye Mola wa walimwengu na kwamba amewapa neema mbalimbali. Wajibu wao ilikuwa kutubia Kwake, kumsadikisha Mtume Wake ambaye ni Swaalih, kumtii katika yale aliyokuja nayo na wasiwatii wapotevu na waeneza ufisadi katika ardhi. Lakini hata hivyo hawakujali nasaha na maelekezo haya. Kinyume chake wakaendelea katika ukaidi wao, upotevu wao na kufuru yao mpaka Allaah akawaangamiza kwa radi na umeme. Tunamuomba Allaah afya. Allaah (Subhaanah) ameeleza vilevile kuhusu kipenzi Wake wa karibu ambaye ni Ibraahiym (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) baadhi ya sifa Zake na kwamba aliwatajia nazo watu wake ili waweze kutubia kwa Allaah, wamuabudu na kumuadhimisha Yeye pale aliposema katika Suurah "as-Shu´araa´":

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ إِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا تَعْبُدُونَ قَالُوا نَعْبُدُ أَصْنَامًا فَنَظَلُّ لَهَا عَاكِفِينَ قَالَ هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ أَوْ يَنفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ

"Wasomee habari za Ibraahiym alipomwambia baba yake na watu wake: "Mnaabudu nini?" Wakasema: "Tunaabudu masanamu, na tutaendelea kuyakalia kwa kuyaabudu." Akasema: "Je, yanakusikieni wakati mnayaomba au yanakunufaisheni au yanakudhuruni?"" (26:69-73)

Tutasimamia hapa. Kwa haya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anawabainishia ya kwamba masanamu hayo hayasilihi kuabudiwa. Kwa kuwa hayasikii na wala hayamuitikii yule mwenye kuyaomba. Vilevile hayanufaisha na wala hayadhuru. Kwani masanamu hayo ni vitu visivyokuwa na uhai. Isitoshe hayawezi kuhisi ile haja ya wenye kuyaomba na yale matatizo walionayo. Ni vipi basi yataombwa badala ya Allaah? Kwa ajili hii amesema:

هَلْ يَسْمَعُونَكُمْ إِذْ تَدْعُونَ أَوْ يَنفَعُونَكُمْ أَوْ يَضُرُّونَ

"Je, yanakusikieni wakati mnayaomba au yanakunufaisheni au yanakudhuruni?"" (26:72-73)

Nini walijibu? Walishindwa kujibu. Wanatambua kuwa waungu hawa hawawezi kunufaisha wala kudhuru na wala hawazisikii du´aa za waombaji na wala hawawaitikii. Kwa ajili hii wakasema:

بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَٰلِكَ يَفْعَلُونَ

“Tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo.” (26:74)

Hawakusema kuwa yanasikia, yananufaisha au yanadhuru. Walishindwa kujibu, jambo ambalo linafahamisha kuchanganyikiwa na kuwa na mashaka. Bali walifikia wao wenyewe kukubali ya kwamba waungu hawa hawastahiki kuabudiwa. Hapo ni pale waliposema:

بَلْ وَجَدْنَا آبَاءَنَا كَذَٰلِكَ يَفْعَلُونَ

“Tumewakuta baba zetu wakifanya hivyo.” (26:74)

Bi maana tulifuata njia na mwenendo wao pasi na kutazama yale tunayoambiwa. Hii ndio maana ya maneno Yake katika Aayah nyingine:

إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَارِهِم مُّقْتَدُونَ

“Hakika sisi tumewakuta baba zetu juu ya dini na hakika sisi ni wenye kufuata nyao zao.” (43:23)

Hii ndio njia na mwenendo wao uliolaaniwa walioufuata na wakatumia kama hoja. Tunamuomba Allaah usalama. Halafu Ibraahiym (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawaambia:

قَالَ أَفَرَأَيْتُم مَّا كُنتُمْ تَعْبُدُونَ أَنتُمْ وَآبَاؤُكُمُ الْأَقْدَمُونَ فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِّي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Akasema: “Je, mnaona hivyo mlivyokuwa mkiviabudu nyinyi na baba zenu waliotangulia? Basi hakika hao ni adui zangu isipokuwa Mola wa walimwengu.”” (26:75-77)

Anakusudia wale waungu wao katika masanamu. Kwa ajili hiyo akasema:

قَالَ أَفَرَأَيْتُم مَّا كُنتُمْ تَعْبُدُونَ أَنتُمْ وَآبَاؤُكُمُ الْأَقْدَمُونَ فَإِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِّي إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“Akasema: “Je, mnaona hivyo mlivyokuwa mkiviabudu nyinyi na baba zenu waliotangulia? Basi hakika hao ni adui zangu isipokuwa Mola wa walimwengu.”” (26:75-77)

Maneno Yake:

إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“... isipokuwa Mola wa walimwengu.””

yanatuthibitishia ya kwamba (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa anajua kuwa wanamuabudu Allaah na wakati huo huo wanaabudu pamoja Naye wengine. Kwa ajili hiyo ndio maana akamvua Mola Wake kwa kusema:

إِلَّا رَبَّ الْعَالَمِينَ

“... isipokuwa Mola wa walimwengu.””

Kama ilivyokuja katika Aayah nyingine:

إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي

“... isipokuwa Yule ambaye ameniumba... ” (43:27)

Ndipo ikapata kujulikana kuwa washirikina walikuwa wakimuabudu Allaah na wakati huo huo wakiabudu pamoja Naye wengine. Ugomvi uliokuwa kati ya wao na Mitume wao ilikuwa katika kumtakasia Allaah ´ibaadah na kumpwekeshea nayo pasi na wengine wote. Kisha baada ya hapo akasema katika kubainisha sifa za Mola:

الَّذِي خَلَقَنِي فَهُوَ يَهْدِينِ وَالَّذِي هُوَ يُطْعِمُنِي وَيَسْقِينِ وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ وَالَّذِي يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحْيِينِ

“Ambaye ameniumba Ndiye aniongozaye, na ambaye Ndiye anayenilisha na ananinywesha; na ninapokuwa mgonjwa, basi Yeye ndiye huniponyesha, na ambaye atanifisha halafu atanihuisha.” (21:78-81)

Haya ndio matendo ya Mola (Jalla wa ´Alaa). Anawaponya wagonjwa, anawafisha, anawahuisha, anawalisha, anawanywesha, anamwongoza

amtakaye, Yeye ndiye muumbaji na muweza wa kusamehe madhambi na kuzisitiri aibu. Kwa ajili hii ndio maana akawa ni mwenye kustahiki ´ibaadah juu ya waja Wake (Jalla wa ´Alaa) na kubatilika kwa ´ibaadah kwa kila asiyekuwa Yeye. Hawaumbi, hawaruzuku, hawanufaishi, hawadhuru, hawajui mambo yaliyofichikana na hawawezi kwa wale wanaowaomba kuwapa manufaa wala madhara yoyote.

06. Allaah ndiye ananufaisha duniani na kuokoa Aakhirah

Amesema (Subhaanah):

ذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ۚ وَالَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا دُعَاءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا مَا اسْتَجَابُوا لَكُمْ ۖ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُونَ بِشِرْكِكُمْ

“Huyo ndiye Allaah, Mola wenu - ufalme ni Wake pekee. Na wale mnaowaomba badala Yake hawamiliki hata kijiwavu cha kokwa ya tende. Mkiwaomba, hawasikii maombi yenu na hata wakiyasikia, hawatakuitikieni na siku ya Qiyaamah watakanusha ushirikina wenu.” (35:13-14)

Akabainisha kutokuweza kwao na kwamba yale maombi yao badala ya Allaah ni shirki. Kwa ajili hii akasema:

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُونَ بِشِرْكِكُمْ

“... na siku ya Qiyaamah watakanusha ushirikina wenu.” (35:14)

Akabainisha (Subhaanah) kutokuweza kwa waungu hawa wote na kwamba kwa haya maombi wamemshirikisha Allaah (´Azza wa Jall). Amesema:

وَالَّذِي أَطْمَعُ أَن يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ

“Na ambaye natumai atanisamehe makosa yangu siku ya Malipo.” (26:82)

Bi maana natumai ya kwamba (Subhaanah) atanisamehe makosa yangu siku ya Qiyaamah. Kwani hakika Yeye (Subhaanah) ndiye mwenye kunufaisha duniani na kuokoka Aakhirah. Kuhusu masanamu haya hayanufaishi si duniani wala huko Aakhirah. Kinyume chake yanadhuru. Kwa ajili hii amesema kuhusu kipenzi Wake wa karibu Ibraahiym:

وَالَّذِي أَطْمَعُ أَن يَغْفِرَ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ رَبِّ هَبْ لِي حُكْمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ وَاجْعَل لِّي لِسَانَ صِدْقٍ فِي الْآخِرِينَ وَاجْعَلْنِي مِن وَرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيمِ

”Na ambaye natumai atanisamehe makosa yangu siku ya Malipo. Mola wangu! Nitunukie hekima na unikutanishe na waja wema, na nijaalie

kusifika kwa wema kwa vizazi vitavyokuja huko baadaye na nijaalie miongoni mwa warithi wa Pepo ya neema." (26:82-85)

Yote haya yanathibitisha kuamini siku ya Mwisho, kuita katika hilo na kuwazindua waja juu ya kwamba kuna Aakhirah ambayo ni lazima ndio itakuwa mwisho wa watu na kwamba kuna malipo na hesabu. Ndio maana akasema baada yake:

وَاجْعَلْنِي مِن وَرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيمِ وَاغْفِرْ لِأَبِي إِنَّهُ كَانَ مِنَ الضَّالِّينَ

"Na nijaalie miongoni mwa warithi wa Pepo ya neema na msamehe baba yangu - hakika yeye amekuwa miongoni mwa waliopotea." (26:85-86)

Alimuombea msamaha kabla ya kujua hali yake. Alipoijua hali yake akajitenga naye mbali.

07. ´Ibaadah ni haki ya Allaah peke yake

Amesema katika Suurah "al-´Ankabuut":

وَإِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاتَّقُوهُ ۖ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ إِنَّمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَوْثَانًا وَتَخْلُقُونَ إِفْكًا ۚ إِنَّ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ لَكُمْ رِزْقًا فَابْتَغُوا عِندَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ وَاشْكُرُوا لَهُ ۖ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

"Ibraahiym pindi alipowaambia watu wake: "Mwabuduni Allaah na mcheni – hakika hivyo ni kheri kwenu mkiwa mnajua. Hakika mnaabudu badala ya Allaah masanamu na mnazua uzushi. Hakika wale mnaowaabudu badala ya Allaah hawakumilikiini riziki, basi tafuteni kutoka kwa Allaah riziki na mwabuduni Yeye na mshukuruni - Kwake ndiko mtarejeshwa."" (29:16-17)

Akabainisha (Subhaanahu wa Ta´ala) ya kwamba ´ibaadah ni haki Yake, kwamba ni wajibu kuogopwa na kuabudiwa Yeye na kwamba waliyoyafanya ni dhambi isiyokuwa na msingi wowote na kwamba waungu wao hawamiliki riziki juu yao kamwe. Vilevile masahamu haya hayawanufaishi wala kuwadhuru na kitu. Hawawamilikii riziki. Allaah (Jalla wa ´Alaa) ndiye Mwingi wa kuruzuku. Ndio maana akasema:

فَابْتَغُوا عِندَ اللَّهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوهُ

"Basi tafuteni kutoka kwa Allaah riziki na mwabuduni Yeye."

Allaah (Subhaanah) ndiye mwenye kuabudiwa na riziki inatafutwa kutoka Kwake (Jalla wa ´Alaa) badala ya wengine wote:

وَاشْكُرُوا لَهُ ۖ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ

"... na mshukuruni - Kwake ndiko mtarejeshwa.""

Yeye ndiye mwenye kurejelewa. Naye (Subhaanah) ndiye mfalme wa kila kitu, muweza wa kila kitu na mwenye kustahiki kushukuriwa kwa ukamilifu wa neema na wema Wake. Yeye ndiye ambaye riziki inatafutwa kutoka Kwake (Jalla wa ´Alaa). Kwa ajili hii amesema katika Aayah nyingine:

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

“Hakika Allaah ndiye Mwingi wa kuruzuku, Mwenye nguvu madhubuti.” (51:58)

وَمَا مِن دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۚ كُلٌّ فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ

“Hakuna kiumbe chochote kitembeacho katika ardhi isipokuwa riziki yake iko kwa Allaah na anajua mahali pake pa kustakiri na pa kuhifadhiwa kwake - yote yamo katika Kitabu kinachobainisha.” (11:06)

Aayah zinazothibitisha kuwa Allaah amewaamrisha Mitume Wake kuwaelekeza waja Wake Kwake na wawajulishe juu ya muumbaji wao, mruzukaji wao na mungu wao ni nyingi sana. Aayah hizo zinapatikana katika Qur-aan. Atakayeizingatia Qur-aan atayakuta hayo yamewekwa wazi na kubainishwa. Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) ndio watu walio wafaswaha na wanaomtambua Allaah zaidi. Vilevile ndio watu walio na uchangamfu zaidi katika kulingania Kwake. Hakuna walio na subira katika kulingania, wanaomjua Allaah zaidi na kuwatakia watu uongofu zaidi kuliko wao. Kwa ajili hii ndio maana wamefikisha ujumbe wa Allaah kwa njia iliokuwa bora na kamilifu zaidi na wakawabainishia watu sifa za muumbaji mwenye haki ya kuabudiwa na majina na matendo Yake (Subhaanah). Waliyapambanua hayo ili waja wamtambua Mola wao na wamjue kwa majina na sifa Zake na haki Yake kubwa juu ya waja Wake. Lengo lingine ni ili vilevile watubie Kwake kwa ujuzi na utambuzi.

08. Muusa na Haaruun walivyotumwa kumlingania Fir´awn

Allaah amesema kuhusu Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na watu wake:

وَإِذْ نَادَىٰ رَبُّكَ مُوسَىٰ أَنِ ائْتِ الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ قَوْمَ فِرْعَوْنَ ۚ أَلَا يَتَّقُونَ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَخَافُ أَن يُكَذِّبُونِ وَيَضِيقُ صَدْرِي وَلَا يَنطَلِقُ لِسَانِي فَأَرْسِلْ إِلَىٰ هَارُونَ وَلَهُمْ عَلَيَّ ذَنبٌ فَأَخَافُ أَن يَقْتُلُونِ قَالَ كَلَّا ۖ فَاذْهَبَا بِآيَاتِنَا ۖ إِنَّا مَعَكُم مُّسْتَمِعُونَ فَأْتِيَا فِرْعَوْنَ فَقُولَا إِنَّا رَسُولُ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Mola wako alipomwita Muusa kwamba: “Nenda kwa watu madhalimu: watu wa Fir’awn, hivi kweli hawamchi Allaah?” Akasema: “Mola wangu! Hakika mimi nakhofu wasije kunikadhibisha na kinadhikika kifua changu na wala ulimi wangu haukunjuki vizuri, hivyo basi basi mtume Haaruun. [Isitoshe wao] wana kisasi juu yangu, basi nakhofu wasiniue.” Akasema: “Hapana! Nendeni kwa alama Zetu, hakika Sisi tu pamoja nanyi Wenye kusikiliza.” Mwendeeni Fir’awn na mseme: “Hakika sisi ni Mitume wa Mola wa walimwengu.”” (26:10-16)

Amewaamrisha awabainishie ya kwamba yeye ni mjumbe wa Mola wa walimwengu. Pengine kwa kufanya hivo wakapata kuzingatia na kurudi katika haki. Lakini hata hivyo hawakupata kuzingatia. Bali waliyapa mgongo yote hayo na wakasema:

قَالَ أَلَمْ نُرَبِّكَ فِينَا وَلِيدًا وَلَبِثْتَ فِينَا مِنْ عُمُرِكَ سِنِينَ وَفَعَلْتَ فَعْلَتَكَ الَّتِي فَعَلْتَ وَأَنتَ مِنَ الْكَافِرِينَ قَالَ فَعَلْتُهَا إِذًا وَأَنَا مِنَ الضَّالِّينَ فَفَرَرْتُ مِنكُمْ لَمَّا خِفْتُكُمْ فَوَهَبَ لِي رَبِّي حُكْمًا وَجَعَلَنِي مِنَ الْمُرْسَلِينَ وَتِلْكَ نِعْمَةٌ تَمُنُّهَا عَلَيَّ أَنْ عَبَّدتَّ بَنِي إِسْرَائِيلَ قَالَ فِرْعَوْنُ وَمَا رَبُّ الْعَالَمِينَ قَالَ رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۖ إِن كُنتُم مُّوقِنِينَ قَالَ لِمَنْ حَوْلَهُ أَلَا تَسْتَمِعُونَ قَالَ رَبُّكُمْ وَرَبُّ آبَائِكُمُ الْأَوَّلِينَ قَالَ إِنَّ رَسُولَكُمُ الَّذِي أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۖ إِن كُنتُمْ تَعْقِلُونَ

“Akasema: “Je, hatukukulea kwetu ukiwa mtoto na ukaishi kwetu miaka mingi ya umri wako na ukafanya kitendo chako ambacho ulikifanya nawe ni miongoni mwa wenye kukosa shukurani.” Akasema: “Nilikifanya hapo wakati nilikuwa miongoni mwa waliokosea. [Lakini] nikakukimbieni nilipokukhofuni na Mola wangu akanitunukia hikmah na akanijalia ni miongoni mwa Mitume - na hiyo ni neema unayonisimbulia kuwa umewatia utumwani wana wa Israaiyl.” Fir’awn Akasema: “Kwani ni nani huyo Mola wa walimwengu?” Akasema: “Mola wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake mkiwa ni wenye yakini.” Akawaambia waliomzunguka: “Je, hivi hamsikilizi kwa makini?” Akasema: “Mola wenu na Mola wa baba

zenu wa awali." Akasema: "Hakika Mtume wenu ambaye ametumwa kwenu bila ya shaka ni mwendawazimu." Akasema: "Mola wa mashariki na magharibi na vilivyo baina yake, mkiwa nyinyi ni wenye kutia akilini."" (26:18-28)

Tazama namna ambavyo Muusa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anawabainishia sifa za Mola (Jalla wa ´Alaa) na kwamba Yeye ndiye Mola wa walimwengu, Mola wa mbingu, Mola wa ardhi na vilivyomo ndani yake, Mola wa viumbe wote na Mola wa mashariki na magharibi. Lengo ni ili adui huyu wa Allaah aweze kurejea katika haki na usawa. Lakini Allaah alikuwa ameshatangulia kujua kuwa ataendelea juu ya upindukaji wake, upotevu wake na kwamba atakufa juu ya ukafiri na ukaidi wake. Tunamuomba Allaah afya. Allaah akambainishia Haaruun na Muusa ya kwamba anawasikia na anawaona na kwamba atawahifadhi, atawanusuru na kuwapa nguvu. Ndio maana akayasambaratisha madai ya mkaidi, mjeuri na mwenye kiburi aliyesema:

فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ

"Akasema: "Mimi ni mola wenu mkuu."" (79:24)

Akawalinda na akawahifadhi kutokamana na shari na njama zake. Hapana shaka kuwa yote haya ni Allaah kuwahifadhi na kuwaangalia Mitume na Manabii wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam).

Fir´awn alikuwa ni mjeuri, mwenye kiburi, mfalme kafiri na mwenye kulaaniwa ambaye anadai kuwa ni Mola wa walimwengu. Pamoja na haya akampa kipaumbele kumlingania na kumbainishia haki ya Allaah juu yake na kwamba ni wajibu kwake kutubia kwa Allaah. Lakini akakataa na kufanya kiburi. Kisha akawaita wachawi wakiume na wakike na mambo kama hayo. Matokeo yake Allaah akabatilisha njama zake na akadhihirisha kutokuweza kwake na akamnusuru Muusa na Haaruun (´alayhimaas-Swalaatu was-Salaam) dhidi ya wale wachawi. Alipoendelea katika upindukaji wake mwisho wake Allaah akamwangamiza yeye na wanajeshi wake wote ndani ya bahari na akamsalimisha Muusa na Haaruun na wana wa israaiyl waliokuwa pamoja nao. Hizi ni mfano wa Aayah za Allaah ambapo Allaah anawalipizia

kisasi na kuwanusuru mawalii Wake dhidi ya maadui Wake. Walikuwa ni watu wawili tu ambao hawakuwa na jengine isipokuwa kundi dogo tu ambao walikuwa watumwa wa Fir´awn aliyekuwa akichinja watoto wao wa kiume na akiwaacha hai wanawake wao na akiwatesa kwa adhabu kali. Wametumwa kwenda kumlingania mfalme mjeuri na mwenye kiburi na kumbainishia haki na kumkatalia ile batili aliyomo. Allaah akawalinda kutokamana na ukandamizaji wake. Sivyo tu bali (Jalla wa ´Alaa) akawafanya imara na akamzungumzisha kwa yale ambayo itakuwa ni hoja dhidi yake. Amesema katika Aayah nyingine:

قَالَ فَمَن رَّبُّكُمَا يَا مُوسَىٰ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ قَالَ فَمَا بَالُ الْقُرُونِ الْأُولَىٰ قَالَ عِلْمُهَا عِندَ رَبِّي فِي كِتَابٍ ۖ لَّا يَضِلُّ رَبِّي وَلَا يَنسَى الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ مَهْدًا وَسَلَكَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا وَأَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِّن نَّبَاتٍ شَتَّىٰ كُلُوا وَارْعَوْا أَنْعَامَكُمْ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي النُّهَىٰ مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ

"Akasema: "Basi ni nani huyo Mola wenu, ee Muusa?" Akasema: "Mola wetu ni Yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza." Akasema: "Basi ni vipi hali ya karne za awali?" Akasema: "Ujuzi wake uko kwa Mola wangu katika Kitabu. Mola wangu hapotezi na wala hasahau; ambaye amekufanyieni ardhi kuwa tandiko na akakupitishieni humo njia na akateremsha kutoka mbinguni maji [ambayo] kwayo Tukatoa aina za mimea mbali mbali. Kuleni na lisheni wanyama wenu - hakika katika hayo kuna ishara kwa wenye akili. Kutokana nayo [hiyo ardhi] Tumekuumbeni na humo tutakurudisheni na kutoka humo tutakutoeni mara nyingine." (20:49-55)

09. Muusa alimweleza Fir´awn ya kwamba Allaah yuko juu mbinguni

Kinacholengwa ni kwamba Mitume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) wamebainisha haki, wakaiweka wazi na wakabainisha majina na sifa za Mola zinazofahamisha uwezo, ukubwa, kustahiki Kwake ´ibaadah na kwamba Yeye ndiye mfalme, mruzukaji, muhuishaji, mfishaji na Mwenye kuyaendesha mambo yote (Jalla wa ´Alaa). Vilevile wakabainisha ujuu wa Allaah na kuwa Kwake juu ya viumbe Wake. Kwa ajili hii Fir´awn alisema kumwambia waziri wake Haamaan:

ابْنِ لِي صَرْحًا لَّعَلِّي أَبْلُغُ الْأَسْبَابَ أَسْبَابَ السَّمَاوَاتِ فَأَطَّلِعَ إِلَىٰ إِلَٰهِ مُوسَىٰ

“Nijengee mnara ili nifikie njia; njia za mbinguni ili nimchungulie Mungu wa Muusa.” (40:37)

Alimweleza kuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) yuko juu ya mbingu. Ndio maana mjeuri huyu akataka kupindukia kwa maneno haya mabaya yasiyokuwa na maana yoyote.

10. Wafuasi wa ´Iysaa wanamtambua Allaah zaidi kuliko Jahmiyyah na vifaranga vyao

Miongoni mwa haya ni yale Allaah (Jalla wa ´Alaa) aliyotaja kuhusu ´Iysaa pamoja na wanusuraji katika Suurah "al-Maaidah" aliposema (Subhaanahu wa Ta´ala):

إِذْ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَن يُنَزِّلَ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِّنَ السَّمَاءِ ۖ قَالَ اتَّقُوا اللَّهَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ قَالُوا نُرِيدُ أَن نَّأْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَن قَدْ صَدَقْتَنَا وَنَكُونَ عَلَيْهَا مِنَ الشَّاهِدِينَ قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنزِلْ عَلَيْنَا مَائِدَةً مِّنَ السَّمَاءِ تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِّأَوَّلِنَا وَآخِرِنَا وَآيَةً مِّنكَ ۖ وَارْزُقْنَا وَأَنتَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ قَالَ اللَّهُ إِنِّي مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ ۖ فَمَن يَكْفُرْ بَعْدُ مِنكُمْ فَإِنِّي أُعَذِّبُهُ عَذَابًا لَّا أُعَذِّبُهُ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ

"Pale waliposema wafuasi watiifu: "Ee 'Iysaa mwana wa Maryam! Je, anaweza Mola wako kututeremshia meza iliyotandazwa chakula kutoka mbinguni?" Akasema: "Mcheni Allaah kama nyinyi kweli ni waumini." Wakasema: "Tunataka kula katika hicho [chakula] na ili nyoyo zetu zitulie na tujue kwamba hakika umetuambia kweli na tuwe juu yake miongoni mwa wanaoshuhudia." Akasema 'Iysaa mwana wa Maryam: "Ee Allaah, Mola wetu, Tuteremshie meza iliyotandazwa chakula kutoka mbinguni ili iwe kwetu ni sikukuu kwa wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu na iwe ni alama itokayo Kwako - hivyo basi Turuzuku, kwani hakika Wewe ni mbora wa wenye kuruzuku." Allaah akasema: "Hakika Mimi nitaiteremsha kwenu, lakini atakayekufuru miongoni mwenu baada ya hapo, basi hakika nitamuadhibu adhabu ambayo sitomuadhibu kwayo yeyote katika walimwengu." (05:112-115)

Katika haya kumebainishwa baadhi ya uwezo wa Allaah (Jalla wa ´Alaa) na kwamba Yeye (Subhaanah) ni muweza wa kila jambo na kwamba Yeye yuko juu. Kwa kuwa kuteremshwa kunakuwa kwa kutokea juu kwenda chini. Kuomba kuteremshiwa chakula yote haya yanathibitisha kuwa watu wake walitambua ya kwamba Mola wao yuko juu. Wao wanamjua na wanamtambua zaidi kuliko Jahmiyyah na vifaranga vyao ambao wamekanusha ujuu. Wanusuraji wamebainisha hilo. ´Iysaa akabainisha hio. Allaah pia kabainisha hilo. Kwa ajili hiyo ndio maana akasema:

إِنِّي مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ

“Hakika Mimi nitaiteremsha kwenu.”

Ni dalili yenye kufahamisha kuwa Mola wetu anaombwa kutoka juu na kwamba yuko juu ya mbingu na juu ya viumbe wote na juu ya ´Arshi. Amelingana juu yake kulingana ambako kunalingana na utukufu na ukubwa Wake. Hafanani (Jalla wa ´Alaa) na viumbe Wake katika sifa Yake yoyote ile.

11. Kuna Aayah nyingi zinazothibitisha kuwa Allaah yuko juu ya mbingu

Kuna Aayah nyingi zinazothibitisha maana hii zenye kuweka wazi kuwa Allaah yuko juu ya viumbe Wake. Miongoni mwazo ni zile Aayah saba zinazojulikana ambapo ndani yake kuna tamko kama lililokuja katika Suurah "al-A´raaf":

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

"Hakika Mola wenu ni Allaah ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya 'Arshi. Anafunika usiku kwa mchana, unaufuatia upesi upesi na jua na mwezi na nyota – vyote vimetiishwa kwa amri Yake. Tanabahi! Ni Vyake pekee uumbaji na amri. Amebarikika Allaah, Mola wa walimwengu." (07:54)

Katika Aayah hii amebainisha ujuu Wake na kwamba Yeye ndiye muumbaji na mruzukaji, kwamba Yeye ndiye mwenye kuumba na kutoa amri (Subhaanahu wa Ta´ala), kwamba anaufunika usiku kwa mchana, kwamba ndiye muumbaji wa jua na mwezi na nyota. Yote haya ili waja waweze kutambua ukubwa wa jambo Lake, ukamilifu wa uwezo Wake, ukamilifu wa elimu Yake (Subhaanah) na kwamba Yeye yuko juu ya viumbe wake wote na ndiye Mwenye kustahiki kuabudiwa (Subhaanahu wa Ta´ala).

12. Baadhi ya sifa za Allaah zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah

Aayah zingine zinazohusiana na maudhui hii ni maneno ya Allaah (´Azza wa Jall):

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ أَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ اللَّهِ ۖ قَالَ سُبْحَانَكَ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي بِحَقٍّ ۚ إِن كُنتُ قُلْتُهُ فَقَدْ عَلِمْتَهُ ۚ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَا أَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّامُ الْغُيُوبِ مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمَرْتَنِي بِهِ أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۖ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنتَ أَنتَ الرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ إِن تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ ۖ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Pindi Allaah atakaposema: “Ee ‘Iysaa mwana wa Maryam! Je, wewe ndiye uliwaambia watu: “Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu miwili badala ya Allaah?” Atasema: “Utakasifu ni Wako! Hainipasi mimi kusema yasiyokuwa haki kwangu, ikiwa nimesema hayo basi hakika Ungeliyajua - Unayajua yale yote yaliyomo katika nafsi yangu na wala mimi sijui yale yaliyomo katika nafsi Yako. Hakika Wewe ni mjuzi wa ghaibu. Sijawaambia lolote isipokuwa yale uliyoniamrisha kwayo kwamba: “Mwabuduni Allaah, Mola wangu na Mola wenu. Nilikuwa juu yao shahidi wakati nilipokuwa nao. Uliponichukua juu, Wewe ndiye ulikuwa mwangalizi juu yao na Wewe juu ya kila kitu ni Mwenye kushuhudia. Ukiwaadhibu, basi bila shaka hao ni waja Wako. Ukiwasamehe, basi hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu kabisa, Mwenye hikmah.” (05:116-118)

Tazama namna anavyobainisha sifa hizi kuu za Allaah (´Azza wa Jall) zinazoita kumuabudu Yeye pekee pasi na wengine wote, kwamba Yeye ndiye mjuzi mkubwa wa vilivyofichikana, kwamba Yeye ndiye Mwenye nguvu kabisa na ndiye Mwenye hekima, kwamba ni Mwenye kuwachunga, kuwaona waja Wake na kwamba anajua yaliyomo katika nafsi ya ´Iysaa ilihali ´Iysaa yeye hajui yaliyomo katika nafsi Yake (Subhaanahu wa Ta´ala). Katika haya kuna dalili ya kuthibitisha sifa na kuonyesha kuwa Mitume wamekuja kuthibitisha majina na sifa za Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanahu wa Ta´ala).

Aidha Yeye (Jalla wa ´Alaa) anasifiwa kuwa na nafsi inayolingana Naye (´Azza wa Jall). Nafsi hii haifanani na nafsi za viumbe. Ni kama ambavyo

Yeye ana uso, mikono, mguu na vidole visivyolingana na sifa za viumbe. Sifa hizo zimethibiti katika Qur-aan na katika Sunnah twaharifu ambapo kumetajwa uso, mikono, vidole na kadhalika.

13. Sifa za viumbe hazifanani na sifa za Allaah kwa njia yoyote ile

Yote hayo yanathibitisha kuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) anasifiwa kwa sifa kamilifu na kwamba hayo hayapelekei kufanana na viumbe Wake. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)

Amejikanushia Mwenyewe kufanana na wakati huo huo akajithibitishia kusikia na kuona. Hayo yanathibitisha kuwa sifa na majina ya Allaah hayana mfano wala cha kulingana nayo. Bali Yeye ni mkamilifu katika dhati, majina, sifa na matendo Yake. Kwa hivyo Yeye (Jalla wa ´Alaa) ndiye anayestahiki kuabudiwa na kuadhimishwa.

Kuhusu viumbe sifa zao ni dhaifu na zina mapungufu. Ama Yeye (Jalla wa ´Alaa) ni mkamilifu katika kila kitu. Ujuzi wake na sifa Zake zingine zote ni kamilifu. Hapana shaka kwamba sifa za viumbe hazifanani na sifa Zake kwa njia yoyote ile. Amesema (Subhaanah):

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

“Basi msimpigie mifano Allaah. Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui.” (16:74)

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ اللَّهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ

“Sema: “Yeye ni Allaah Mmoja pekee. Allaah ambaye ndiye mkusudiwa haja zote. Hakuzaa na wala hakuzaliwa. Na wala hakuna yeyote anayelingana [wala kufanana] Naye.” (112:01-04)

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)

14. Mfumo wa Ahl-us-Sunnah katika kuthibitisha majina na sifa za Allaah

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanathibitisha yale majina na sifa za Allaah zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah Swahiyh kwa njia inayolingana Naye (Jalla wa ´Alaa). Wanafanya hivo pasi na kupotosha, kukanusha, kuzifanyia namna, kuzipigia mfano, kuzidisha wala kupunguza. Bali wanazithibitisha na kuzipitisha kama zilivyotajwa na wakati huo huo wanaamini kuwa ni haki na kwamba zimethibiti kwa Allaah kwa njia inayolingana Naye (Subhaanahu wa Ta´ala) na isiyofanana na viumbe Wake. Amesema (´Azza wa Jall):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)

Haya ni masuala miongoni mwa masuala ya Tawhiyd. Bali ni katika masuala muhimu. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amebainisha majina na sifa Zake katika Qur-aan na akayakariri hayo sehemu nyingi ili ukubwa wa majina, sifa na ukubwa wa matendo Yake uweze kujulikana. Matendo Yake yote ni matukufu, majina Yake yote ni mazuri mno na sifa Zake zote ni kuu. Kwa hayo ndio waja watamtambua Mola wao na matokeo yake wamuabudu kwa ujuzi na watubie Kwake kwa elimu na kwamba anayasikia maombi yao, anawajibia wale wenye dhiki na kwamba Yeye juu ya kila jambo ni muweza.

15. Ndio maana ndama hakustahiki kuabudiwa

Katika haya kunaingia vilevile yale aliyotaja Allaah (Jalla wa ´Alaa) kuhusu watu wa Muusa katika wana wa israaiyl pindi walipomwabudu ndama na akawawekea wazi (Subhaanah) ufisadi wa jambo lao na ubatilifu wa waliyoyatenda. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

وَاتَّخَذَ قَوْمُ مُوسَىٰ مِن بَعْدِهِ مِنْ حُلِيِّهِمْ عِجْلًا جَسَدًا لَّهُ خُوَارٌ ۚ أَلَمْ يَرَوْا أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا يَهْدِيهِمْ سَبِيلًا ۘ اتَّخَذُوهُ وَكَانُوا ظَالِمِينَ

“Watu wa Muusa wakajichukulia, baada ya kuondoka kwake, katika mapambo yao umbo la ndama - ililikuwa na sauti kama ya ng’ombe. Je, hawakuona kuwa huyo [ndama] hawazungumzishi na wala hawaongozi njia? Walimfanya [mungu] na wakawa madhalimu.” (07:148)

Akabainishia kuwa mungu anayestahiki kuabudiwa ni lazima awe ni mwenye kuzungumza, awe ni mwenye kusikia na ni mwenye kuona, awe ni mwenye kuongoa njia, awe ni mwenye uwezo wa wazi na mjuzi juu ya kila jambo. Ama kumuabudu ndama asiyekuwa na uhai badala ya Allaah ni katika kuharibika kwa akili. Ndama asiyemuitikia mwenye kuiomba, hazungumzi, haitiki na hanufaishi na wala hadhuru – ni vipi ataabudiwa badala ya Allaah? Katika Aayah nyingine anasema (Jalla wa ´Alaa):

أَفَلَا يَرَوْنَ أَلَّا يَرْجِعُ إِلَيْهِمْ قَوْلًا وَلَا يَمْلِكُ لَهُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا

“Je, hawaoni kuwa [huyo ndama] harejeshi neno na wala hawezi kuwadhuru na wala kuwanufaisha?” (20:89)

Bi maana ndama huyu hamuitikii yule anayemzungumzisha na wala hamwongeleshi. Aidha hamiliki manufaa wala kudhuru. Ni vipi basi atatekelezewa ´ibaadah iwapo akili za watu hawa zingelikuwa timamu?

16. Ndio maana Allaah akastahiki kuabudiwa

Kuna Aayah nyingi katika Qur-aan zilizo na maana kama hii ambapo Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anawabainishia waja Wake ya kwamba Yeye ndiye anayestahiki kuabudiwa kwa sababu ya ukamilifu wa uwezo Wake, kwamba Yeye ndiye mfalme wa kila kitu na ndiye muweza juu ya kila jambo, kwamba anayasikia maombi ya wenye kuomba, anakadiria kuwatatulia haja zao na anamjibu yule mwenye dhiki katika wao, anamiliki madhara na manufaa na anamwongoza amtakaye katika njia iliyonyooka.

17. Kazi kubwa waliokuwa nayo Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam)

Allaah amemtuma Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ambaye ndiye kiongozi wa viumbe, mbora wao na kiongozi wa Mitume, kwa kazi aliyowatuma kwayo Mitume wengine wa mwanzo katika kulingania katika kumuabudu Allaah peke yake, kumtakasia Yeye ´ibaadah, kulingania katika hayo, kubainishia sifa na majina Yake na kwamba Yeye ndiye anayestahiki kuabudiwa. Kwa hivyo ulinganizi wake ukawa mkamilifu. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: “Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote.”” (07:158)

Akamteremshia Kitabu kikubwa na ndio kitukufu, kikubwa na chenye manufaa zaidi. Amebainishia ndani yake Tawhiyd, kwamba Yeye ndiye Mola mtukufu, muweza wa kila jambo, mfalme wa kila kitu, mwenye kunufaisha na kudhuru. Halafu katika Aayah nyingi akaamrisha kuwafikishia watu hayo. Atakayeizingatia Qur-aan atazijua. Amesema (Subhaanah):

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۚ قُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ

“Ukiwauliza: “Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi?” Watasema: “Allaah.” (31:25)

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

“Sema: “Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini au nani anayemiliki kusikia na kuona na nani anayemtoa aliye hai kutoka maiti na anayemtoa maiti kutoka aliye uhai na nani anayeendesha mambo yote? Watasema: “Ni Allaah”, basi sema: “Je, basi kwa nini hamchi?” (10:31)

Allaah akamwamrisha Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) atumie hoja dhidi yao kwa yale matendo na uwezo wa Mola waliyoyakubali,

kwamba Yeye ndiye mwenye kuhuisha na mwenye kufisha, kwamba Yeye ndiye anayeendesha na Mwingi wa kuruzuku juu ya ile Tawhiyd-ul-´Ibaadah waliyoikanusha na kuipinga.

Anachotaka kusema ni kwamba: ikiwa mnakubali wenyewe ya kwamba huyu ndiye Mola wenu, mmiliki, mwenye kudhuru na mwenye kunufaisha, anayeendesha mambo, muhuishaji, mfishaji na anawaruzuku waja Wake – ni kwa nini basi msiache kumshirikisha na badala yake mkamuabudu pekee pasi na wengine wote? Amesema tena (Subhaanah):

قُل لِّمَنِ الْأَرْضُ وَمَن فِيهَا إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۚ قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ

“Sema: “Ni ya nani ardhi na wale waliokuwemo ndani yake mkiwa mnajua?” Watasema: “Ni ya Allaah pekee.” Sema: “Je, kwa nini hamkumbuki”?” (23:84-85)

Vilevile na Aayah zilizoko baada yake.

Yote haya ni makumbusho kutoka kwa Allaah kwenda kwa waja Wake kupitia kwa Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa ukubwa wa haki Yake, majina na sifa Zake na kwamba Yeye (´Azza wa Jall) ndiye anayestahiki kuabudiwa kwa sababu ya ukamilifu wa uwezo Wake, ujuzi Wake, wema Wake na kwamba Yeye ndiye mwenye kunufaisha na mwenye kudhuru na Yeye ndiye muweza juu ya kila jambo, aliyepwekeka katika matendo, majina na sifa Zake kutokamana na wenza na washirika (Jalla wa ´Alaa).

18. Tawhiyd kwanza

Pindi Allaah alimpomtuma Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alianza Da´wah yake kwa Tawhiyd kwanza. Hivyo ndivyo walivyofanya Mitume wengine waliomtangulia. Aliwaambia Quraysh:

"Enyi watu wangu! Semeni ´hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah` mtafaulu.""[1]

Namna hii ndio alianza. Hakuwaamrisha swalah, zakaah, kuacha pombe, uzinzi na mfano wa hayo. Kinyume chake alianza nao kwa Tawhiyd kwa kuwa ndio msingi. Msingi ukitengemaa mengine yatajengwa juu yake. Akaanza nao kwa msingi mkubwa ambao ni kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye ´ibaadah na kumuamini Yeye na Mitume Wake (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam).

Msingi wa mila na msingi wa dini katika Shari´ah ya kila Mtume ni kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye dini. Kumpwekesha na kumtakasia Allaah dini ndio dini ya Mitume wote na vilevile ndio nafasi ya ulinganizi wao wote na lengo la ujumbe wao wote (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam), kama tulivyotangulia kusema.

[1] Ahmad (03/492).

19. Namna waarabu walivyobadilishiwa dini yao

Wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipowaambia watu wake:

“Semeni “hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah.””[2]

waliyakataa na kuyakemea hayo. Kwa kuwa yanaenda kinyume na yale waliyomo wao na baba zao. Walikuwa juu ya shirki na kuabudu mizimu kwa kipindi kirefu baada ya ´Amr bin Luhay al-Khuzaa´iy kuwabadilishia dini yao ambaye ndiye alikuwa raisi wa Makkah. Imesemekana kuwa alisafiri kwenda Shaam na akawakuta watu wanaabudu masanamu ndipo akarudi Makkah na akawalingania watu kuyaabudu masanamu kwa ajili ya kuwaiga makafiri. Kuna maoni mengine yanayosema vilevile ya kwamba alielekezwa mahali ambapo akaambiwa kuwa kuna masanamu mengi, Wadd, Suwaa´, Yaghuuth, Ya´uuq na Nasr, na akaelezwa awalinganie waarabu kuyaabudu na kwamba yatawajibu. Akaenda sehemu ile kuyafukua na akayaeneza kati ya waarabu ambapo wakayaabudu. Haya ndio yale masanamu yaliyokuwa yakiabudiwa wakati wa Nuuh. Yakajulikana kati ya waarabu na wakayaabudu badala ya Allaah kwa sababu ya ´Amr bin Luhay huyu aliyetajwa. Kisha wakatafuta masanamu na mizimu mingine katika makabila mengine ambayo wakawa wanayaabudu pamoja na Allaah, wakiyaomba kutatua haja, wakiyafanya kuwa ni miungu pamoja na Allaah na wakijikurubisha kwayo kwa sampuli mbalimbali za ´ibaadah kama vile kuyachinjia, kuyaomba, kuyapapasa na mengineyo. Katika hayo ni al-´Uzzaa lililokuwa sanamu la watu wa Makkah, Manaat lililokuwa sanamu la watu wa al-Madiynah na watu wa pembezoni mwake, al-Laat lililokuwa sanamu la watu wa Twaaif na watu wa pembezoni mwake. Kulikuwa pia masanamu na mizimu mingine mingi kati ya waarabu. Wakati Mtume wetu huyu mtukufu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipowalingania katika kumuabudu Allaah peke yake na kujiepusha na waungu wao ndipo wakamkemea na kusema:

أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَهًا وَاحِدًا ۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ

[2] at-Tirmidhiy (3232) na Ahmad (01/228).

“Amewafanya waungu wote hawa kuwa ni mungu Mmoja? Hakika hili ni jambo la ajabu mno!" (38:05)

Amesema (Jalla wa ´Alaa) kuhusu wao katika Suurah “as-Swaaffaat”:

إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ وَيَقُولُونَ أَئِنَّا لَتَارِكُو آلِهَتِنَا لِشَاعِرٍ مَجْنُونٍ

“Hakika wao walipokuwa wakiambiwa: “Hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah” hutakabari na wanasema: “Je, sisi kweli tuache waungu wetu kwa ajili ya mshairi mwendawazimu?”” (37:36)

20. Mtume na Maswahabah wake kuhajiri al-Madiynah kukimbia maudhi ya Quraysh

Ndugu! Tazama namna ujinga ulivyosheheni kwao mpaka wakafanya wito wa kulingania katika Tawhiyd ni jambo la ajabu, wakaukataa, wakashangazwa nao, kumfanyia uadui yule mwenye kulingania katika hayo mpaka wakafikia kumpiga vita na mwishowe wakaafikiana wote kumuua. Hatimaye Allaah akamuokoa kutokamana na njama zao na (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akahajiri kati yao kuelekea al-Madiynah. Kisha wakajaribu kumuua tena siku ya Badr lakini hawakufaulu. Halafu wakajaribu hayo siku ya Uhud zaidi kuliko walivyojaribu hapo kabla lakini Allaah akamtosheleza na njama na vitimbi vyao. Kisha wakajaribu tena siku ya Ahzaab kutokomeza wito, Mtume na Maswahabah wake lakini Allaah akasambaratisha njama zao na Allaah akamuokoa kutokamana na shari na vitimbi vyao, akainusuru dini yake, akatia nguvu wito wake, akamsaidia juu ya kupambana na maadui wake mpaka Allaah akampumbaza macho yake kabla ya kufa kwake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa kushinda dini ya Allaah, kuenea haki, Tawhiyd ya Allaah kuenea ardhini, kutokomeza mizimu na masanamu baada ya Allaah kuufungua mji wa Makkah katika mwaka wa 8 tangu kuhajiri katika mwezi wa Ramadhaan. Watu wakaingia katika dini ya Allaah wakiwa makundi kwa makundi kwa sababu ya Allaah kumfungulia mji wa Makkah na Quraysh pia wakaingia katika Uislamu. Vilevile makabila mengine yakafuatia kuingia katika Uislamu na kukubali kumuabudu na kumtakasia ´ibaadah Allaah (Jalla wa ´Alaa) pekee na kushikamana barabara na Shari´ah Yake, mambo ambayo yalikuwa yakilinganiwa naye (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

21. Chanzo cha kujitokeza shirki na kubainisha kwamba Nuuh ndiye Mtume wa kwanza

Kinacholengwa ni kwamba Mtume na Nabii wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alilingania katika yale waliyolingania kwayo Mitume wengine kabla yake kuanzia Nuuh na wengine waliokuja baada yake ambapo ilikuwa kulingania katika kumuabudu Allaah peke yake na kumtakasia Yeye ´ibaadah na kuacha kuabudu vyengine badala Yake. Huu ndio ulikuwa wito wake wa kwanza na ndio ilikuwa wajibu muhimu zaidi na wajibu mkubwa zaidi.

Wana wa Aadam walikuwa katika Tawhiyd tokea wakati wa Aadam mpaka wakati wa Nuuh (´alayhis-Salaam) kwa muda wa karne ishirini. Hivyo ndivyo alivyosema Ibn ´Abbaas na wengineo. Walipotofautiana kwa sababu ya shirki iliyotokea kwa watu wa Nuuh ndipo Allaah akamtuma Mtume. Amesema (Jalla wa ´Alaa):

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّينَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ

“Watu walikuwa ummah mmoja kisha Allaah akatuma Manabii wakiwa ni wabashiriaji na waonyaji.” (02:213)

Maana yake ni kuwa watu walikuwa Ummah mmoja katika Tawhiyd na imani na wakatofautiana baada ya hapo. Amesema katika Aayah nyingine katika Suurah “Yuunus”:

وَمَا كَانَ النَّاسُ إِلَّا أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

“Watu hawakuwa isipokuwa ni ummah mmoja halafu wakakhitilafiana. Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako, bila shaka ingehukumiwa baina yao katika yale waliyokuwa kwayo wakikhitilafiana.” (10:19)

Maana yake ni kwamba walikuwa katika Tawhiyd na imani. Haya ndio maoni ya haki. Halafu baada ya hapo wakatofautiana kwa sababu ya shaytwaan kuwaita katika kumuabudu Wadd, Suwaa´, Yaghuut, Ya´uuq na Nasr. Kulipotokea shirki kwa watu wa Nuuh kwa sababu ya kupetuka kwao kwa

watu wema na shaytwaan akawapambia ´ibaadah ya asiyekuwa Allaah ndipo Allaah akamtuma Nuuh (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) ambapo akawalingania katika kumuabudu na kumtakasia ´ibaadah Allaah pekee na kuepuka kuabudu asiyekuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye akawa Mtume wa kwanza aliyetumwa na Allaah kwa watu wa ardhini baada ya kujitokeza shirki ndani yake. Kuhusu Aadam kuna Hadiyth zimepokelewa zinazofahamisha kuwa yeye ni Nabii na Mtume aliyezungumzishwa, lakini hata hivyo hazitegemewi kwa sababu ya udhaifu wa mlolongo wa wapokezi wake. Hapana shaka kuwa (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) aliteremshiwa Shari´ah kutoka kwa Mola wake na kizazi chake kilikuwa juu ya Shari´ah, kumuabudu na kumtakasia ´ibaadah Allaah peke yake. Halafu baada ya hapo kwa karne kumi au alizotaka Allaah ndipo kukatokea shirki kwa watu wa Nuuh kwa Wadd, Suwaa´, Yaghuuth, Ya´uuq na Nasr kama tulivyotangulia kusema.

Imepokelewa katika mapokezi yanayojulikana kutoka kwa Ibn ´Abbaas na wengineo ya kwamba Wadd, Suwaa´, Yaghuut, Ya´uuq na Nasr walikuwa ni watu wema. Walipokufa ndipo shaytwaan akawapa ilhamu watu wake watengeneze katika vikao vyao picha zao na wawaite kwa majina yao ambapo wakafanya hivo. Pindi walipokufa na elimu ikasahaulika ndio wakaabudiwa badala ya Allaah (´Azza wa Jall). Wakati elimu ilipopotea na wanachuoni wakawa wachache ndipo shaytwaan akawajia watu na kuwaeleza namna ambavyo masanamu hayo yametengenezwa kwa sababu yalikuwa yananufaisha, kuombwa, kutakwa uokozi na kuombwa mvua. Mwishowe shirki ikatokea kwa sababu hiyo. Kwa hapa inapata kutambulika kuwa Nuuh (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndiye Mtume wa kwanza aliyetumwa na Allaah kwa watu wa ardhini baada ya kujitokeza kwa shirki.

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea ya kwamba watu wataokuwa wamesimama siku ya Qiyaamah watamwendea Nuuh na kumwambia: “Ee Nuuh! Wewe ndiye Mtume wa kwanza uliyetumwa na Allaah kwa watu wa ardhini. Tushufaie kwa Mola wako[3].

[3] al-Bukhaariy (3340), Muslim (194) na at-Tirmidhiy (2434).

22. Idadi ya Mitume na Manabii haitambuliki

Kuhusu Aadam (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) umethibiti utume wake kabla ya hapo kwa dalili zingine kukiwemo yale yaliyopokelewa katika Hadiyth ya Abu Dharr kupitia kwa Abu Haatim bin Hibbaan na wengineo ya kwamba alimuuliza (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu Mitume na Manabii ambapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Manabii 124.000 na Mitume ni 313." Katika upokezi wa Abu Umaamah imekuja: "Ni 315". Lakini hata hivyo zote mbili ni Hadiyth dhaifu kwa mujibu wa wanachuoni. Zina yenye kuyatia nguvu lakini hata hivyo pia ni dhaifu, kama tulivyotoka kutaja punde tu. Katika baadhi ya mapokezi hayo yanasema kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema: "Ni Manabii 1.000 na zaidi." Mapokezi mengine yanasema: "Manabii ni elfu tatu." Hadiyth zote zilizokuja juu ya mada hii ni dhaifu. Bali Ibn-ul-Jawziy ameizingatia Hadiyth ya Abu Dharr ni katika Hadiyth zilizotungwa. Kinachotakwa kusemwa ni kwamba hakuna katika idadi ya Mitume na Manabii mapokezi yenye kutegemewa. Hakuna yeyote anayejua idadi yao isipokuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Lakini ni kundi la maelfu. Allaah ametusilimulia visa vyao baadhi yao na wala hakutusimulia visa vya baadhi ya wengine kwa sababu ya hekima Yake kubwa. Faida kubwa ni sisi tujue kuwa wote walilingania katika kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye ´ibaaah na kwamba waliwalingania watu wao katika hayo. Miongoni mwao kuna waliokubali wito huo, kuna wengine walioukataa, baadhi walikubali baadhi ya mambo na kuna wengine walikataa yote. Hivyo ndivyo alivyoeleza Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

23. Maudhi yaliyompata Mtume na watu wake kwa sababu ya Tawhiyd

Yametambulika yale magomvi na mizozo iliyompitikia Mtume wetu, ambaye ndiye wa mwisho wao na mbora wao (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), yeye pamoja na watu wake Makkah. Hakika aliudhiwa sana yeye na Maswahabah wake mpaka wakaafikiana kumuua. Hatimaye Allaah akamuokoa kati yao. al-Madiynah zilipitika vita na Jihaad kuu mpaka Allaah akamnusuru na akampa nguvu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa hayo inapata kuwabainikia wote ya kwamba wito wa Mitume wote ilikuwa kulingania katika kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye ´ibaadah na kwamba Manabii na Mitume wote walilingania katika kumpwekesha Allaah na kumtakasia Yeye ´ibaadah, kuamini majina na sifa Zake na matendo Yake, kwamba Yeye (Subhaanah) amepwekeka katika uola Wake, majina na sifa Zake na kustahiki Kwake kuabudiwa pasi na wengine wote. Hakuna mwengine yeyote anayeistahiki asiyekuwa Yeye. Ni mamoja akawa ni Mtume, Malaika, mja mwema na viumbe wengine wote. ´Ibaadah ni haki ya Allaah (Jalla wa ´Alaa). Kwayo ndio (Subhaanahu wa Ta´ala) ameumba viumbe. Kwayo amewatuma Mitume. Amesema (Subhaanah):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

“Sikuumba majini na wanadamu isipokuwa waniabudu.” (51:56)

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)

24. Lengo la kuteremshwa Vitabu

Mitume wametumwa na Vitabu vimeteremshwa kwa sababu ya kumuabudu na kumpwekesha Allaah. Amesema (Ta´ala):

كِتَابٌ أُحْكِمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِن لَّدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ

“Kitabu ambacho Aayah Zake zimetimizwa barabara kisha zikapambanuliwa kutoka kwa Mwenye hikmah, mjuzi - kwamba: “Msiabudu mwengine isipokuwa Allaah.”” (11:01-02)

هَٰذَا بَلَاغٌ لِّلنَّاسِ وَلِيُنذَرُوا بِهِ وَلِيَعْلَمُوا أَنَّمَا هُوَ إِلَٰهٌ وَاحِدٌ وَلِيَذَّكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ

”Huu ni ufikisho kwa watu na ili wawaonye kwayo na ili wapate kujua ya kwamba hakika Yeye ndiye mwabudiwa wa haki mmoja na ili wakumbuke wale wenye akili.” (14:52)

Allaah ameweka wazi katika Qur-aan kupitia Aayah Zake na viumbe Wake yanayothibitisha juu ya uwezo Wake mkubwa, uungu na uola Wake na kwamba Yeye ndiye anayestahiki kuabudiwa. Atayezingatia Kitabu cha Allaah na viumbe Wake basi ataona kupitia alama zinazosomwa, zenye kuhisiwa na maelezo yenye kunakiliwa yanayothibitisha ya kwamba Yeye ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa na kwamba Mitume wote wamefikisha na kulingania katika hayo na kwamba shirki iliyojitokeza kwa watu wa Nuuh bado ipo mpaka hii leo. Wapo katika watu wanaoyaabudu masanamu, mizimu na kupetuka kwa watu wema na Manabii ambao wanawaabudu pamoja na Allaah. Hilo linatambulika na yule anayefuatilia khabari za ulimwenguni tokea wakati wa Nuuh mpaka hii leo.

25. Uchambuzi wa aina za Tawhiyd

Kutokana na yale tuliyotaja kutoka katika Qur-aan, maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na uhalisia wa ulimwengu basi itabaini kuwa Tawhiyd imegawanyika aina mbalimbali. Hayo yamejulikana na wanachuoni kupitia tafiti za kisomo ya Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Tawhiyd imegawanyika aina tatu:

1- Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah: Ni kuamini kuwa Allaah amepwekeka katika matendo Yake, uumbaji Wake na kwamba Yeye ndiye mwenye kuwaendesha waja vile anavyotaka kwa ujuzi na uwezo Wake (Jalla wa ´Alaa).

2- Tawhiyd-ul-Asmaa´ was-Swifaat: Ni kuamini kuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni mwenye kusifiwa kwa majina mazuri mno na sifa kuu, kwamba Yeye ni mkamilifu katika dhati Yake, majina Yake, sifa Zake na matendo Yake na kwamba Yeye hana mwenza wala mshirika.

3- Tawhiyd-ul-´Ibaadah: Ni kuamini kuwa Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ndiye anayestahiki kuabudiwa peke, hali ya kuwa hana mshirika, pasi na wengine wote. Ukipenda pia unaweza kusema kuwa kumpwekesha Allaah ni kule kuamini ya kwamba Yeye ndiye Mola wa wote, muumba wa wote, anayewaruzuku wote na kwamba hana mshirika katika matendo Yake yote (Subhaanahu wa Ta´ala). Kwa msemo mwingine hana mshirika katika kuumba na kuwaruzuku Kwake waja. Hana mshirika katika kuyaendesha Kwake mambo. Yeye ndiye mfalme wa kila kitu. Amesema (Subhaanah):

لِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا فِيهِنَّ ۚ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Ni wa Allaah pekee ufalme wa mbingu na ardhi na yale yote yaliyomo humo. Naye juu ya kila jambo ni muweza.” (05:120)

Yeye ndiye mfalme wa kila kitu na mwenye kukiendesha kila kitu (Jalla wa ´Alaa). Amri zote ni Zake. Uumbaji wote ni Wake. Amesema (Ta´ala):

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ

“Tanabahi! Ni Vyake pekee uumbaji na amri.” (07:54)

Yeye ni mwenye kusifiwa kwa sifa kamilifu na ni mwenye kuitwa kwa majina mazuri. Hana mshirika kutoka katika viumbe Wake kwa chochote. Bali Yeye ni mkamilifu katika dhati Yake, majina Yake, sifa Zake na matendo Yake. Yeye ndiye mwenye kustahiki kuabudiwa na kukhusishwa kwa ´ibaadah kukiwemo du´aa, khofu, matarajio, utegemezi, shauku, woga, swalah, swawm, kichinjwa, nadhiri na mengineyo. Yote haya yanaingia katika neno "Tawhiyd". Tawhiyd ya Allaah (Subhaanah) ni ile Tawhiyd ya Manabii na Mitume. Tawhiyd ya Allaah ni ile aliyokuja nayo wa mwisho wao na kiongozi wao, Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Tunaweza vilevile kuigawanya kwa ibara nyingine na kusema kuwa Tawhiyd ya Allaah waliyokuja nayo Mitume wote imegawanyika sehemu mbili:

1- Tawhiyd fiyl-Ma´arifah wal-Ithbaat: Maana yake ni kuamini majina, sifa za Allaah, dhati ya Allaah (Jalla wa ´Alaa), kuwaumba Kwake viumbe, kuwaruzuku na kuyaendesha mambo yao. Huku ndio kupwekesha katika utambuzi na kuthibitisha. Kwa msemo mwingine ni kwamba unatakiwa kuamini na kusadikisha ya kwamba Allaah (Subhaanah) amepwekeka katika uola Wake, majina na sifa Zake na kuwaendesha Kwake waja, kwamba Yeye ndiye muumbaji wao, mruzukaji wao na mwenye kusifiwa kwa sifa kamilifu zilizotakasika na mapungufu na kasoro. Yeye hana mshirika, mwenza wala yeyote anayelingana Naye (Jalla wa ´Alaa) katika hayo.

2- Tawhiyd-ul-Qaswd wat-Twalab: Ni kumpwekesha Allaah (Subhaanah) katika makusudio yako, maombi yako, swalah yako, swawm yako na ´ibaadah zako zingine zote. Usimkusudie katika hayo mwengine isipokuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa). Vivyo hivyo swadaqah zako na matendo yako mengine yote unayojikurubisha kwayo usimkusudie mwengine isipokuwa Yeye pekee. Usimwombe mwengine asiyekuwa Yeye. Usimuwekee nadhiri mwengine asiyekuwa Yeye. Usijikurubishe kwa aina mbalimbali za ´ibaadah isipokuwa Kwake. Usimwombe kuwaponya wagonjwa na kutaka nusura dhidi ya maadui isipokuwa kutoka Kwake. Unatakiwa kumpwekesha katika hayo hayo.

Hizi ndio aina za Tawhiyd. Unaweza kueleza kuwa kuna aina mbili, aina tatu au aina moja kama tulivyotangulia kutaja hivi punde. Hakuna mgongano

katika istilahi na ibara hizo. Muhimu ni wewe kutambua ni Tawhiyd sampuli gani ambayo Allaah amewatuma Mitume, akateremsha Vitabu na kukatokea mizozo kati ya Mitume na watu wao kwa ajili yake. Nayo si nyingine ni Tawhiyd-ul-´Ibaadah.

26. Msimamo wa washirikina wa kale na wa sasa juu ya Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah

Mitume na watu wao hawakugombana kitendo cha Allaah kuwa ndiye Mola wa wote, kawaumba wote, anawaruzuku wote, kwamba ni mkamilifu katika dhati Yake, majina Yake, sifa Zake, matendo Yake, kwamba hana mshirika, mwenza na anayelingana Naye. Washirikina wote wa Qurayash na hata wengine walikuwa ni wenye kuyakubali. Yaliyotokea kwa Fir´awn kupinga na kudai kuwa yeye ndiye mungu ilikuwa tu kwa ajili ya jeuri yake na wakati huo huo alikuwa akitambua ndani ya nafsi yake kuwa ni batili. Muusa alisema kumwambia:

لَقَدْ عَلِمْتَ مَا أَنزَلَ هَٰؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ بَصَائِرَ

“Hakika umeshajua kwamba hakuna aliyeteremsha haya isipokuwa Mola wa mbingu na ardhi kuwa ni dalili za kuonekana dhahiri.” (17:102)

Amesema (Subhaanah) juu yake na watu mfano wake:

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا

“Wakazikanusha kwa dhulma na majivuno na hali kuwa nafsi zao zimeziyakinisha.” (27:14)

قَدْ نَعْلَمُ إِنَّهُ لَيَحْزُنُكَ الَّذِي يَقُولُونَ ۖ فَإِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُونَكَ وَلَٰكِنَّ الظَّالِمِينَ بِآيَاتِ اللَّهِ يَجْحَدُونَ

“Hakika Tunajua kwamba yanakuhuzunisha yale wanayoyasema. Hakika wao hawakukadhibishi wewe, lakini madhalimu wanazikanusha alama za Allaah.” (06:33)

Kadhalika washirikina wenye kusema kuwa mungu ni mwanga na giza hawakufanya hivo isipokuwa pia ni kwa sababu ya jeuri. Pamoja na hayo hawakusema kuwa wanalingana. Hakuna katika ulimwengu waliosema kuwa kuna waungu wawili wanaolingana katika uendeshaji.

Kuhusu wakanamungu (*atheists*) kumkana Mola wa walimwengu na kupinga kuwepo kwa Qiyaamah sio jambo la kushangaza kutoka kwa maadui wa

Allaah. Hilo ni kwa sababu ya kuharibika kwa akili zao kwa sababu ya kutawaliwa na shaytwaan mpaka akawatoa katika maumbile ya Allaah aliyowaumba kwayo watu wote. Wakanamungu hawa, hata kama wanapinga kwa midomo yao, ndani ya nyoyo zao wanayakubali hayo. Hayo yanakubaliwa hata na vitu visivyokuwa na uhai. Amesema (Subhaanah):

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَاوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَن فِيهِنَّ ۚ وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَٰكِن لَّا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا

"Zinamsabihi mbingu saba na ardhi na vile vilivyomo ndani yake; na hakuna kitu chochote isipokuwa kinasabihi kwa himdi Zake njema, lakini hamzifahamu tasbihi zao. Hakika Yeye ni mpole, Mwingi wa kusamehe." (17:44)

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَمَن فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِّنَ النَّاسِ ۖ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ

"Je, huoni kuwa wanamsujudia Allaah walioko mbinguni na ardhini, na jua, na mwezi na nyota, na majabali na miti na viumbe vinavyotembea na wengi miongoni mwa watu? - na wengi imewastahiki adhabu." (22:18)

Tunachotaka kusema ni kuwa wale makafiri wenye kutenda matendo ya jinai wanaomkana Mola wa walimwengu uhalisia wao ni kuwa ni wenye jeuri juu ya maumbile na akili zao. Hakika maumbile na akili vyote viwili vinathibitisha kuwepo kwa Mola ambaye anauendesha ulimwengu, anayewaendesha waja, asiyekuwa na anayelingana Naye, mshirika wala mwenza – ametakasika na ametukuka kwa yale wanayosema madhalimu kutakasika kuliko kukubwa. Kwa ajili hii ndio maana tukasema kuwa washirikina [wa Quraysh] waliikubali Tawhiyd-ur-Rubuubiyyah, majina na sifa Zake na hawakuipinga. Walikuwa wakitambua kuwa Allaah (Jalla wa ´Alaa) ndiye aliyewaumba viumbe, mwenye kuwaruzuku, anayeendesha mambo yao, mwenye kuteremsha mvua, mwenye kuhuisha na kufisha kama tulivyotangulia kutaja hapo nyuma.

27. Uwajibu wa kupupia kulingania na kueneza kheri

Ee mja! Ni wajibu kwako baada ya kutambua yaliyotangulia utilie mkazo kueneza msingi huu mkubwa kabisa, kuueneza kati ya watu na kuuweka wazi kwa viumbe ili wautambue wale wasioujua na ili pia wampwekeshe Allaah wale wanaomshirikisha na kwenda kinyume na maamrisho Yake. Vilevile kwa kufanya hivo utakuwa umewafuata Mitume na mfumo wao katika kulingania katika dini ya Allaah na kutekeleza amana uliyobebeshwa. Utakuwa na thawabu sawa na za wale ambao Allaah atakawaongoza kupitia mikono yako mpaka siku ya Qiyaamah. Allaah (´Azza wa Jall) amesema:

وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّن دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ

“Ni nani mwenye kauli nzuri zaidi kuliko yule anayelingania kwa Allaah na akatenda mema na akasema: “Hakika mimi ni miongoni mwa waislamu?”” (41:33)

قُلْ هَـٰذِهِ سَبِيلِي أَدْعُو إِلَى اللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي ۖ وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

“Sema: “Hii ndio njia yangu nalingania kwa Allaah juu ya ujuzi: mimi na anayenifuata. Utakasifu ni wa Allaah, nami si miongoni mwa washirikina.”” (12:108)

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۖ وَجَادِلْهُم بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

“Lingania katika njia ya Mola wako kwa hikmah na mawaidha mazuri na jadiliana nao kwa ambayo ni mazuri zaidi.” (16:125)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema katika Hadiyth Swahiyh:

“Atakayefahamisha kheri, basi ana mfano wa ujira wa yule mtendaji.”[4]

Ameipokea Muslim katika “as-Swahiyh” yake.

Alisema kumwambia ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) pindi alipomtuma Khaybar:

[4] Muslim (1893), at-Tirmidhiy (2671), Abu Daawuud (5129) na Ahmad (04/120).

“Ninaapa kwa Allaah! Allaah kukuongozea mtu mmoja tu ni bora kwako kuliko ngamia wekundu.”[5]

Ameipokea al-Bukhaariy na Muslim.

Mpaka hapa. Ninamuomba Allaah (´Azza wa Jall) awawafikishe wote juu ya kujifunza dini Yake, kunyooka katika yale yanayomridhisha, atukinge sote kutokamana na sababu zinazopelekea katika ghadhabu Zake na mitihani inayopotosha. Ninamuomba vilevile (Subhaanah) ainusuru dini Yake, aliweke juu neno Lake, azitengeneze hali za waislamu na awatawalishie wale wabora wao. Hakika Yeye (Subhaanahu wa Ta´ala) ni Mwingi wa kutoa, mkarimu. Himdi zote anastahiki Allaah, Mola wa walimwengu.

Swalah na salaam zimwendee mja na Mtume Wake; Mtume wetu Muhammad, kizazi chake, Maswahabah wake na wale watakaowafuata kwa wema mpaka siku hiyo ya Mwisho.

[5] al-Bukhaariy (3701), Muslim (2406), Abu Daawuud (3661) na Ahmad (05/333).